wa Meli Tanzania (TASAC) limewahikikishia mawakala binafsi wa meli kuwa litafanya shughuli zake kwa mujibu wa sheria iliyopo na halitaingilia shughuli zinazopaswa kufanywa na watu binafsi kama wengine wanavyodhania na kulalamikia uwepo wake.

Mhandisi Emmanuel Ndomba alisema kuwa TASAC imeundwa kwa mujibu wa sheria na haijawekwa kwa ajili ya kufuta mawakala wengine bali ni kusimamamia shughuli za meli kwa uhakiki na usalama zaidi.

Aliongeza kuwa mpaka kushughulikia kazi zote nne walizopewa kwa mujibu wa sheria ambap watakuwa wanashughu meli zote za kijeshi,

# Wanufaika mradi wa ufugaji kuku

**Na Allan Ntana, Igunga**

JUMLA ya vikundi 45 vya wakulima vyenye wanachama wapatao 960 vimeundwa katika Kata ya Mbutu wilayani Igunga Mkoani Tabora na kunufaika kupitia utaratibu wa kupeana zawadi ulioanzishwa na mradi wa EPOG (Exponential Pass on the Gift).

Akizungumza katika hafla iliyoandaliwa na Shirika la Heifer International Tanzania juzi katika kata hiyo, mwezeshaji wa vikundi hivyo, Athanas Mbugashida alisema kuwa mradi huo unatekelezwa na shirika hilo katika kata mbili za Mbutu na Igunga wilaya humo.

Alisema kuwa ujio wa mradi huo imekuwa neema kwa wananchi wa hali ya chini kwani wengi wao hawakuwa na uwezo wa kupata mtaji wa kuanzisha mradi wa ufugaji kuku na mingineyo lakini kupitia mradi huo wamepata kuku wa kufuga.

Mbugashida alifafanua kuwa awali walikuwa na vikundi 10 tu kijijini hapo vilivyokuwa na jumla ya watu 250 lakini baada ya kupewa mafunzo na wataalamu wa mradi huo walifanikiwa kuongeza idadi hiyo hadi kufika vikundi 43 vyenye watu 960 na wote ambao hawakuwa na kuku walipewa na wenzao.

Alibainisha kuwa utekelezwaji wa mradi huo kwa vitendo umeleta neema kubwa sana kwa wananchi kwani awali walikuwa na kuku wapatao 7,567 tu lakini baada ya kupewa elimu na kufuata mwongozo wa mradi sasa wana kuku 19,394.

Mbugashida aliongeza kuwa mbali na elimu ya ufugaji bora waliyopewa na kupeana zawadi,pia walipewa mafunzo ya kilimo bora,ujasiriamali na utunzaji mazingira na wameweza kupanda miti zaidi ya 4000 katika kata hiyo.

Aidha alisisitiza kuwa kupitia mradi huo wameweza kupata teknolojia ya majiko banifu ambayo hutumia kuni kidogo sana hivyo kuepusha tabia ya ukataji miti ovyo ambao hupelekea uharibifu wa mazingira.

Meneja Mafunzo wa Shirika hilo, John Toto alisema kuwa mafanikio yaliyopatikana kupitia mradi huo ni mfano wa kuigwa na wananchi wa kata nyingine ambazo hazikufikiwa na mradi huo katika wilaya hiyo.

Naye Kaimu Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Shadrack Pastory aliwahakikishia wananchi wa kata hiyo kuwa hata kama mradi huo utaisha watasimamia ipasavyo yale yote yaliyoanzishwa na Shirika hilo ili yaendelee kuwanufaisha wananchi.


UZA, NUN
KUTA

**VIWANJA**
Vinauzwa vipo mae Tabata, Mbagala, T Msasani, Salasala, Mabwepande na m mengine.
**Simu:** 06832466

**NYUMBA**
Inauzwa iko Tabat st.Mary ina vyumb master, nyuma ku 2 ina hati miliki be 90 pia viwanja vin Goba ukubwa mit kingine 30x25 bei
**Simu:** 07150275

**ENEO**
Linauzwa liko Kin Mtenga ukubwa eka moja bei ni n maelewano yapo
**Simu:** 0718611

**VIWANJA**
Vinauzwa viko V ukubwa 50x40 2,000,000 milic
**Simu:** 071502

**NYUMBA**
Inauzwa iko Ma iko kwenye kon 500 maelewar
**Simu:** 068324

**NYUMBA**
Inauzwa ina fre na kupanga zi maeneo ya Ka Mikocheni, M Salasala, Gob

Bidhaa........
Maelezo......
Mawasilian


Scanned by CamScanner

ka mgonjwa

# kwa kulu

akiwapigia simu watu na
ia ujumbe mfupi wa maandishi
adhi yao, akiwaaminisha yeye
manda wa Polisi Mkoa wa
na kuwaeleza amepatwa na
a kijamii na kuwataka washiriki
changia fedha au vitu, huku
zingira aliyopo hawezi kuongea
ne pesa au watumie ujumbe
vasiliana nae," alisema Muliro.

**GA WA JADI ALIYEMBAKA A**

huo huo, Jeshi la Polisi
wanza, linamshikilia mganga
Hemed Jumanne (40), mkazi
ema, akituhumiwa kumbaka
wake (jina linahifadhiwa).
a huyo
wa kumbaka mwanamke
wenye umri wa miaka 32,
utimba, wilayani Nyamagana.
da Muliro alisema tukio hilo
nuari 4, mwaka huu, saa 1:00
atika Mtaa wa Jiwe, Kata ya
a ya Nyamagana.
alisema kuwa siku ya tukio,
wa tukio hilo alikwenda
nga huyo kupata tiba ya
yanayomsumbua, ndipo
yo aliingiwa na tamaa ya
a baadae alimpa dawa za
a.
jibu wa Muliro, muathirika
va hospitali na hali yake
vizuri na kuruhusiwa. Alitoa
kwa wananchi kujiepusha
i ya wahalifu wanaotumia
uganga wa jadi kutapeli watu
vitendo vingine vya kijinai.



# nto

hemu, Ihucha Jumanne,
hakuonekana nyumbani
na haikujulikana alipo,
a na watu akiwa amekufa
nbeni mwa mto Irisya.
a ya Ikungi, Edward
harisha wananchi kuwa
i yao kutokana na mvua
sasa na kusababisha
vidimwi, kujaa maji na
a watu, hususan watoto.
a Uhuru, Mpogolo
a hali ya hewa mwaka
epo kwa mvua kubwa
emba, mwaka jana hadi
aarifa za baadhi ya watu
yo ni vyema kuchukua

# Udhibiti uvuvi haramu waongeza upatikanaji samaki

**SUPERIUS ERNEST**

WAVUVI wanaofanya shughuli za uvuvi katika Bahari ya Hindi, ijini Dar es Salaam, wameipongeza serikali inayoongozwa na Rais Dk. John Magufuli, kwa kudhibiti uvuvi haramu kwani umefanikisha ongezeko la upatikaji wa samaki.

Akizungumzia kudhibitiwa kwa uvuvi huo, Said Ahmad, ambaye ni mvuvi anayeuza samaki katika Soko la Feri, lililoko Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam, alisema udhibiti huo kupitia sheria ya kuzuia uvuvi haramu umekuwa na tija kubwa.

"Uvuvi haramu wa kutumia baruti na makokolo ulikuwa unaharibu sana samaki, lakini tangu uzuiwe, samaki wanapatikana kwa wingi tofauti na siku za nyuma.

"Nawashauri waliokuwa wanatunia uvuvi haramu waache kuilaumu serikali kwa kusema imeondoa ajira, bali wajue fursa bado ipo, wanaweza kujiunga na wenzao, ambao wanafanya uvuvi halali na kujipatia riziki kwa wasaa zaidi," alisema.

Athumani Sabuni, ambaye ni mvuvi maarufu wa dagaa katika soko hilo, aliiomba serikali kutolegeza kamba katika kusimamia udhibiti wa uvuvi haramu.

**"Uvuvi haramu wa kutumia baruti na makokolo ulikuwa unaharibu sana samaki, lakini tangu uzuiwe, samaki wanapatikana kwa wingi tofauti na siku za nyuma.**

Mvuvi wa dagaa, Soko la Feri, Athumani Sabuni

"Nashauri sheria ya udhibiti wa uvuaji haramu iendele kusimamiwa kweli kweli. Viongozi ambao wanaisimamia waendelee kukaza kabisa ili waliokuwa wanatumia njia hiyo wasije wakarudia," alisema.

Kwa upande wake, Mwajuma Moyo Ofisa Uvuvi wa Soko la Feri, alisema wanaendelea kuwa makini kuhakikisha hakuna samaki waliovuliwa kwa mabomu wanaoingia sokoni hapo.

"Sisi Manisapaa ya Ilala hatuna eneo la kuvua, lakini tunajua kwa asilimia 90 uvuvi wa kutumia baruti umepungua , sasa tunaendelea kupambana na tatizo la uvuvi wa kutumia makokoro," alisema.

Alisema wanaendelea kufanya doria za mara kwa mara, ambapo Desemba, 20 mwaka jana, walifanikiwa kukamata mitumbwi mitatu yenye makokoro.

Aliwataka wavuvi kuzingatia ukataji wa leseni kwa ajili ya kuendelea na shughuli yao hiyo na kuepusha usumbufu wowote dhidi yao.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi na Ufugaji kutoka Wizara ya Mifugo, Magese Bulai, aliwataka wavuvi kuendelea kufuata sheria za uvuvi endelevu wa kutumia zana halali.

Scanned by CamScanner